JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS MAENDELEO YA VIJANA (OR-MV)

TANGAZO LA FURSA YA MIKOPO KUPITIA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA

Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana (OR-MV) inautangazia umma, hususan vijana wote nchini, kuwa dirisha la kupokea maombi ya mikopo kupitia **Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF)** limefunguliwa rasmi. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeanzishwa na Serikali kwa lengo la kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mitaji ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za uzalishaji, biashara na utoaji wa huduma. Kupitia mfuko huu, Serikali inalenga kukuza ujasiriamali, kuongeza fursa za ajira na kujiajiri kwa vijana, pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa. Hivyo, vijana wenye sifa wanahimizwa kutumia fursa hii kwa kuwasilisha maombi yao kwa kuzingatia vigezo na taratibu zilizowekwa za kupata mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

1 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 35.

ii. Awe na barua ya uthibitisho kutoka Serikali ya Mtaa au Kijiji atakapofanyia biashara au kutekeleza mradi wake.

iii. Mwombaji anaweza kuwa mtu binafsi, kampuni changa inayoanza au kikundi cha kijamii kilichosajiliwa na kinachojihusisha na shughuli za kiuchumi.

iv. Waanzilishi wa vikundi au kampuni za vijana wanaoomba mkopo wasiwe waajiriwa katika sekta rasmi (Serikalini au sekta binafsi).

v. Kikundi au kampuni inayoomba mkopo iwe tayari kuzingatia na kutekeleza sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia utoaji wa mikopo.

2 NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI YA MKOPO

i. Mwombaji anatakiwa kuwa amejisajili katika Mfumo wa Uwezeshaji Vijana (YES) kupitia tovuti ya **portal.vijana.go.tz.**

ii. Kabla ya kuwasilisha ombi la mkopo, mwombaji anatakiwa kuhakikisha kuwa amekamilisha kujaza taarifa zote za wasifu wake katika Mfumo wa YES kwa asilimia 100.

iii. Mwombaji anatakiwa kufuata kwa usahihi maelekezo yanayotolewa kupitia Mfumo wa YES wakati wa kuwasilisha ombi la mkopo.

3 VIAMBATISHO MUHIMU VYA MAOMBI YA MKOPO

i. Mwombaji awe na barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa au Kijiji atakapotekeleza shughuli zake za biashara au mradi.

ii. Mwombaji mwenye biashara inayoendelea awe na nakala ya cheti cha usajili wa biashara kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

iii. Mwombaji awe na nakala ya uthibitisho wa namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

4 TAREHE YA MWISHO YA KUTUMA MAOMBI YA MKOPO

Tangazo hili limetolewa **tarehe 30 Oktoba 2026,** mwisho wa kupokea maombi ya mkopo ni **tarehe 28 Novemba 2026, saa 5:59 usiku (23:59).** Waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Mfumo wa YES kupitia tovuti ya **portal.vijana.go.tz.** na kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa ndani ya muda uliotangazwa. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu hayatafanyiwa kazi.

Limetolewa na;

KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - MAENDELEO YA VIJANA
MJI WA SERIKALI, MTUMBA – DODOMA